



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI.

KIKAO KAZI CHA 4 CHA SERIKALI MTANDAO 2024

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

**Ndugu Wanahabari,**

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) inatarajia kufanya Kikao Kazi cha 4 cha Serikali Mtandao kuanzia Februari **6-8, 2024** katika Ukumbi wa AICC – jijini Arusha. Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora **Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb)**.

Takriban wadau **1500** wa Serikali Mtandao kutoka katika Mashirika na Taasisi za Umma wakiwemo Maafisa Masuuli, Wakuu wa Vitengo vya TEHAMA, Maafisa TEHAMA, Maafisa Rasilimali watu, Maafisa Mipango, Maafisa Mawasiliano, Wahasibu pamoja na Watumiaji wote wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini wanatarajiwa kushiriki.

Lengo la kikao kazi hicho ni kuwakutanisha wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao, ili kujadiliana juu ya mafanikio, changamoto pamoja na kuweka mikakati mbalimbali ya kukuza Serikali Mtandao nchini, ili kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya TEHAMA katika Taasisi za Umma; sambamba na kuboresha utendaji kazi katika taasisi hizo ili kuwezesha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

**Ndugu Wanahabari,**

Serikali Mtandao ni matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji kazi wa taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa umma. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ndiyo taasisi iliyopewa jukumu la kuratibu, kusimamia na kukuza juhudi za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza uzingatiwaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika Taasisi za umma ili kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya TEHAMA yanazingatiwa katika Taasisi hizo.

Katika kutekeleza majukumu yake, Mamlaka hushirikiana na wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao katika kukuza juhudi za Serikali Mtandao nchini. Miongoni mwa juhudi hizo ni pamoja na kukutana na wadau hao kupitia Vikao Kazi vya Serikali Mtandao vinavyoandaliwa na Mamlaka.

Aidha, Kikao Kazi cha 4 cha Serikali Mtandao kinaongozwa na kaulimbiu isemayo **“Uzingatiaji wa Sheria, Sera, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa ubadilishanaji Salama wa Taarifa.”** Falsafa ya Kaulimbiu hii ni kuhamasisha ubadilishanaji salama wa taarifa kupitia mfumo wa **GovESB** (*Government Enterprise Service Bus*).

### **Ndugu Wanahabari,**

Tukumbuke kwamba, Mamlaka ya Serikali Mtandao imetekeleza agizo la **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan**, la kutaka mifumo yote ya TEHAMA Serikalini inawasiliana na kubadilishana taarifa. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imetekeleza agizo la **Mhe. Rais** kwa kusanifu na kutengeneza mfumo huo wa Ubadilishanaji taarifa Serikalini yaani **Government Enterprise Service Bus -GovESB**.

Hadi sasa, taasisi za umma **109** zimeunganishwa katika mfumo huu, na mifumo **117** imesajiliwa na kubadilishana taarifa. Katika kikao kazi cha nne cha Serikali Mtandao, washiriki wataweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kila taasisi ya umma inazingatia Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika ujenzi wa mifumo na miradi ya TEHAMA, ili mifumo hiyo iweze kusomana na kubadilishana taarifa kadri itakavyohitajika.

Aidha, Mamlaka imejipanga kuweka mwelekeo wa Serikali Mtandao katika miaka ijayo kwa kuandaa na kutekeleza mikakati madhubuti ili Serikali Mtandao ifikie kuwa na:

- i. Sehemu moja ambayo huduma mtandao zote zitakuwa zinapatikana.
- ii. Uwezo wa kutumia teknolojia mpya zinazoibuka, hasa zile za akili bandia, sarafu za kidijiti n.k, ili kuwezesha maboresho ya kiutendaji katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa umma.
- iii. Vijana wa kitanzania wenye uwezo mkubwa wa ubunifu katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.
- iv. Mifumo na miundombinu ya Serikali Mtandao iliyo bora na imara zaidi.
- v. Ubadilishanaji kamili wa taarifa miongoni mwa mifumo tumizi ya kitaasisi na kisekta ya Serikali Mtandao.
- vi. Uwezo mkubwa wa kudhibiti matishio ya usalama mtandaoni.
- vii. Namba moja ya utambuzi kurahisisha utoaji wa huduma mtandao kwa umma.

**Ndugu Wanahabari,**

Mamlaka ya Serikali Mtandao inatoa rai na kuwakumbusha wadau wote wa TEHAMA hapa nchini kushiriki kikamilifu katika Kikao **kazi cha 4 cha Serikali Mtandao**.

**#KaributuijengeSerikaliKidijitali#**

**Imetolewa Na:**



**Mha. Benedict Ndomba**

**MKURUGENZI MKUU**

**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**